# Lihubiri
# Neno
# Katika
# Wagalatia

**Na Andrew M. Connally**

**Kimetolewa Na:**
**Chimala School of Preaching**
**P.O. Box 724**
**Mbeya, Tanzania**

**www.kanisalakristo.com**

# Yaliyomo


| Somo: | Uka: |
|---|---|
| 1. Hatari YaWagalatia | 3 |
| 2. Makanisa Ya Galatia | 6 |
| 3. Injili Moja | 8 |
| 4. Injili Iliyofunuliwa | 10 |
| 5. Injili Moja Iliyofunuliwa Imejaribiwa | 12 |
| 6. Kusulibiwa Pamoja Na Kristo | 14 |
| 7. Roho Mtakatifu - Kwa Njia Ya Imani Au Torati | 16 |
| 8. Ahadi - Sheria - Na Injili | 18 |
| 9. Fumbo La Sara Na Hajiri | 20 |
| 10. Uhuru Katika Kristo | 22 |
| 11. Matendo Ya Mwili (1) | 24 |
| 12. Matendo Ya Mwili (2) | 25 |
| 13. Matendo Ya Mwili (3) | 27 |
| 14. Roho Na Tunda Lake | 28 |
| 15. Kurejeza Anayepotea | 30 |
| 16. Kupanda Na Kuvuna | 32 |
| 17. Huwezi Kumdanganya Mungu | 34 |
| 18. Msalaba Wa Kristo | 36 |

# Hotuba Kutoka Katika Wagalatia

## HATARI YA WAGALATIA

Azimio: Hatari ya Wagalatia ilihusiana na maiundisho ya Kiyahudi na mambo ya ulimwengu pia hilo lahusika sana na siku za kizazi chetu hiki.

Shabaha: Kuonyesha sawa sawa picha ya hatari ya Wagalatia.

Dibaji: Tunafikiri kuwa shida na majaribu yetu lea yanatofautiana na yale ya vizazi vilivyopita, lakini kila siku yanakuwa karibu sawa tu. Watu kwa ujumla hawabadiliki kutoka kizazi hadi kingine. Mapigano yetu ya kutunga unyofu wa kanisa na usafi wa roho zetu wenyewe ni karibu sawa na siku zile za Paulo.

Baada ya kuanzisha makanisa katika Galatia, mtume alipata kwarnba makanisa hayo yarno katika hatari ya aina mbili ambazo zilifanya kusanyiko kupotoka ikiwa na mafundisho ya Kiyahudi na mambo ya ulimwengu. Maovu haya mawili bado yanaleta tisho kubwa kwa kanisa katika kizazi hiki chetu.

A. Uongofu wa Wagalatia.

1. Paulo aliihubiri injili, ambayo sasa ilikuwa inageuzwa, Wagal. 1: 6-8, ambamo katika hiyo alimwonyesha Kristo aliyesulubishwa, 3:1-2.
2. Maneno haya waliyakubali wakiutii ukweli wake, kwayo walikuwa wana wa Mungu, 3:23-29.
3. Kama wana wa Mungu kwa njia ya ukombozi kwa njia ya mbegu ya mwanamke walikuwa warithi wa Mungu na warithi pamoja na Kristo, Wagal. 4:4-7; War. 8:14-17.
4. Walianza vizuri, lakini sasa walianza kuzuiliwa na waalimu waongo waliokuja miongoni mwao, 5: 7.
5. Uhuru, usafi na unyofu wa kanisa ulianza kuhatarishwa kutoka sehemu mbili: mafundisho ya waalimu waongo wa Kiyahudi na mambo ya ulimwengu, yaani, dhambi za tamaa, ambazo ziliweza kuharibu imani yao. Hizi zinahatarisha kanisa hata leo, na chochote kinacho hatarisha kanisa kinatuhatarisha wewe na mimi tulio kanisa.

B. Hatari ya Kwanza: Tisho la Mafundisho ya Kiyahudi.

1. Mafundisho ya waalimu waongo yalikuwa ni ugeuzo wa injili, hakuna injili nyingine, 1:6-10, ilikuwa ni "kuwaloga" wasikilizaji, 3:1.
2. Kristo aliwakomboa kutokana na laana ya torati, iIikuwa katika ahadi ya kiroho kwa lbrahimu kwamba Mataifa watabarikiwa, 3:8-14.
3. Ndani ya Kristo walifanywa huru, uhuru kutokana na utumwa kwa torati na dhambi, 5:1.
4. Mwalimu mpya wa uongo alikazia juu ya tohara akifuatanisha na ukristo, lakini hili basi, liliwafanya kuwa wadeni katika torati yote iIiyoamriwa, 5:2-3.

5. Lakini kutafuta kuhesabiwa haki kwa njia ya sheria, iwapo ni kwa shabaha moja au zote, ilikuwa ni kutengwa na Kristo, 5:4-6.

C. Hatari ya Mafundisho ya Kiyahudi Leo.

1. Tohara sio shabaha leo, Iakini mafundisho ya Kiyahudi bado yanatoa tisho hili.

2. Namna yoyote ya kurudia torati na kuruhusu zoezi lo lote la kidini, ni kurudia katika mafundisho ya Kiyahudi, kama vile ilivyokuwa tohara.

a. Wa Seventh-Day Adventist wanashikiIia utunzaji wa Sabato. Hii ni ya Torati.

b. Agano la watoto wachanga uhusiano wao na Mungu, ambao unatafutwa na ubatizo wa watoto wachanga ni kurudia katika mambo ya sheria ya kimwili badala ya mambo ya kugeuka kiroho kwa moyo wa mtu.

c. Vinanda vya muziki katika ibada havina mamlaka nyingine zaidi kuliko ile ya Musa, hata hivyo Kristo lazima atoe mamlaka juu ya mazoezi yote ya kidini leo, Math. 28:18; Wakol. 13:17.

d. Utawala wa Miaka Elfu - imani ya kwamba Kristo atarudi duniani na kuanzisha Ufalme wa kidunia kwa miaka elfu moja ni aina ya mafundisho ya Kiyahudi yanayopatikana katika madhehebu. Kristo ni mfalme sasa, Mdo. 2: 29-36; Ufalme wake na Kanisa, Math. 16:16-18; na wakristo wa awali walikuwa katika Ufalme, Wakol. 1:13. Wakristo wanatawala pamoja na Kristo katika maisha haya sasa, War. 5: 17. Yesu anaketi katika mkono wa kuume wa Mungu akiamuru na kutawala kama Nabii, Kuhani na Mfalme, Waebr. 1:1-14. Yesu atatawala mpaka mauti imekomeshwa, 1 Wakor. 15: 25·28.

e. Hao wanaoamini uongo wa utawala wa miaka elfu moja wanatazamia jambo sawa na Iile ambalo Wayahudi walilitazamia katika siku za Kristo. Kwa kuamini hivyo ni kurudisha mafundisho ya Kiyahudi na torati, Paulo analipinga hili kabisa kabisa na daima, 2 Wakor. 5:l6-17.

D. Tisho la Pili: Hatari ya Mambo ya Ulimwengu.

1. Uhuru ndani ya Kristo haukuwa wa kuinua matakwa ya mwili: lIiwabidi Wagalatia wajifunze hili, ndivyo inavyotupasa nasi leo, 5:13.

2. Matendo ya mwili yalikuwa na ni yenye kuangamiza maisha ya kiroho ya mkristo, 5:16-24.

3. Mambo ya ulimwengu huleta tisho linaloendelea la upotovu; linaanza kwa "kutokuona maumivu" katika jambo na kuishia katika maangamizo, Wagal. 6:7-8; watu wengine "hawaoni maumivu," kwa sababu ni vipofu kiroho, Waebr. 5:12-14.

4. Dhambi zile zile zilizokuwa "matendo ya mwili," wakati ule na majaribu kwa wanadamu ni "matendo ya mwili" sasa, 5:19-20, na huishia na amri ile ile, "kwamba watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu," 5:21-

E. Tibabu la Mungu kwa Hatari ya Wagalatia.

1. Kataa kunaswa katika mambo ya jinsi hiyo, 5:1.

2. Uenende kwa kufuata Raha, 5:16.

3. "Usulibishwe pamoja na Kristo," Wagal. 2:20; 5:24.

4. Uone fahari katika msalaba, 6:14.
5. Raya ndiyo matibabu yetu leo!

Mwisho: Tusidhani ya kuwa tumeshapita hatari ya siku za awali. Hali ya wanadamu haijabadilika, wala shetani. Majaribu kila siku yapo. lbilisi anabadilisha majaribu kulingana na hali mpya tu. Tisho kila siku lipo, akingoja kudanganya wasiojali.
Ahadi ya baraka ya kiroho katika mbegu ya Ibrahimu imetimizwa, sasa utakuwa mwana wa Mungu kwa njia ya imani kwa kuutii ukweli wa injili? Ni mwaliko wa Mungu kwamba ufanye hivyo.

## MAKANISA YA GALATIA

Azimio: Makanisa ya Galatia yalianzishwa na Paulo akiihubiri injili. Sasa walikuwa katika hatari ya kuanguka kutoka katika neema kwa sababu ya mafundisho ya uongo waliyokuwa wan ayaamini na kujizoeza.

Shabaha: Kuonyesha jinsi injili ilivyopandwa katika Galatia na ni jambo gani lililokuwa linatokea baina ya makanisa.

Dibaji: Ni jambo geni kwamba Paulo hakuandika barua kwenye makanisa yaliyoanzishwa wakati wa safari yake ya kwanza, lakini hata moja iliyomfikia. Aliwatembelea akirejea nyumbani pamoja na Barnaba, Mdo. 14:21-23. Aliwatembelea tena katika safari yake ya pili na Sila, Mdo. 16:1-2.

Kwa kujifunza makanisa ya Agano Jipya twaweza kujifunza masomo ya maana kwa ajili ya kanisa la Agano Jipya la siku hizi.

A. Kuanzishwa kwa Makanisa ya Galatia.

1. Galatia lilikuwa jimbo la Rumi, likifanywa. hivyo na Agosto Kaisari, 25 K K. Watu walikuwa wa vizazi vya Wagauli, walioivamia nchi katika karne ya tatu K. K.
2. Wakaaji wa nchi walikuwa wenye kugeuka-geuka katika hali; kama tunavyojifunza kihistoria tu, bali pia na katika barua aliyowaandikia Paulo.
3. Mahubiri yaloyofanywa kwanza katika jimbo yaliyokuwa ya Paulo na Sila katika safari ya pili, Mdo. 16:6; ambayo ilitokana na kuugua kwa Paulo, Wagal. 4:13-14; War. 8:28.
4. Barua ya Paulo haikuandikwa kwa kusanyiko moja rasmi, lakini kwa kusanyiko lote la "makanisa ya Galatia," Wagal. 1: 2-3. Hakuna jiji rasmi, la Galatia lililotajwa.

B. Ukombozi Wao: Fundisho Walilolipokea.

1. Wakati Paulo alipowatembelea kwanza na kuhubiri, walikuwa chini ya utumwa kwa "miungu," Wagal. 4:8.
2. Paulo aliwahubiri injili, aliyoipokea kwa Kristo, Wagal. 1:6-12.
3. Katika maneno haya Yesu Kristo aliwekwa wazi mbele zao, Wagal. 3:1; 1 Wakor. 15:1-4; yakizaa imani, Wagal. 3:2.
4. Lakini sasa kwa kuwa wengine walikuwa wakidanganywa na waalimu waongo kuhusu torati na injili, ilimbidi kuweka mstari ulio wazi kati ya ahadi ya imani na torati, 3:6-14.
5. Baraka zikiwa kwa njia ya ahadi, zilizo za imani, si kwa torati, ingekuwa vingine, wokovu ungekuwa wa torati, 3:16-21.
6. Torati ilikuwa ni kiongozi tu kuwaleta kwa Kristo, ambaye kwake walihesabiwa haki kwa njia ya imani, Wagal. 3:23-25.
7. Sasa wamekuwa wana wa Mungu si kwa njia ya Ibrahimu katika mwili, lakini kwa njia ya ahadi iliyofanyika kwa Ibrahimu kwa njia ya imani ndani na katika ubatizo ndani ya Kristo, 3: 26-29, ambao ulikuwa sawa na huduma ya Yesu, Mk. 16:15-16.

8. Ndani ya Kristo, sasa walikuwa wana wa Mungu, wakiburudika na baraka kamili za ushirika huo, na pia wana wa Ibrahimu kwa njia ya imani 3:29; 4:45; War. 8:14-17.

C. Maisha Yao: Mafundisho Yenye Adili Waliyokuwa Wakliyapokea.

1. Rata hivyo katika Kristo na mbegu ya Ibrahimu, waliweza kuanguka kutoka kwenye neema kurudia katika mafundisho ya Kiyahudi, Wagal. 5:4. (Mtu hawezi kutengwa na kitu ambacho hakuunganishwa nacho - waliweza kuanguka kutoka katika neema!)
2. Pia lazima watambue kwamba mambo ya sherehe tu, au imani peke yake haikuweza, lazima iwe inayotenda kwa njia ya upendo, 5:6.
3. Lazima waliwahakikishia mambo ya uadilifu, na vile vile ya mafundisho, kisha, wao, lazima waenende kwa njia ya Roho, 5:16-18.
4. Matendo ya mwili yanaweza, na yataweza leo, kumzuia mtu mbinguni, 5:19-21. Ichunguze kila dhambi, na namna kila mkristo anavyotakiwa daima kupigania kunyenyekea chini ya Roho.
5. Lakini tunda la Roho liko na hao waliosulibiwa pamoja na Bwana, na wameusulibisha mwili, 5:22-24.
6. Maisha haya yenye adili lazima yajionyeshe katika kuishi hasa, kutenda merna, ili mmoja awe na mahali pa kuvuna, 6:6-10.

Mwisho: Makanisa yalianzishwa juu ya mahubiri ya injili; wasikilizaji walioamini walizidishwa kwa Kristo kwa njia ya kubatizwa ndani Yake. Maisha yao yalikuwa ya kumwonyesha Kristo, kwa kuusulibisha mwili, na kuishi kwa k.ufuata Roho kwa pando ambalo watavuna maisha ya milele.

Leo tunayatambua makanisa ya Krista katika njia hiyo hiyo. Ukifanya kama walivyofanya utakuwa mshiriki wa kanisa la Kristo sawa na Wagalatia. Huu ni mpango wa Mungu kwako, kwanini usiyaamini mambo haya, uzitii amri zote za injili, ili na wewe pia, uvune maisha ya milele.

**INJILI MOJA**

Wagal. 1:1-5.

Azimio: Kuna injili moja tu ye yote anayetafuta kuibadili au kuigeuza kwa namna yo yote ni mwenye kuigeuza injili ya kweli.

Shabaha: Kumwonyesha mwandishi, mwisho wake, na sababu ya kitabu cha Wagalatia.
Dibaji: Huenda hakuna kitabu kingine kilichofanya kazi munimu katika Urudisho kuliko kitabu cha Wagalatia. Msemo wake wa kuhesabia haki kwa njia ya imani kama vile Iljia ya matendo ya Wakatoliki yalivyomshitua Martin Luther. Kitabu kimefahamika kama "Hati ya Uhuru wa Mkristo."

Somo hili ni dibaji ya kitabu. Ndani yake tunakusudia kuchunguza has a matukio ya maandishi ya kitabu, na tofauti kati ya "injili" na "injiIi iliyo tofauti." Hakuna injiIi "nyingine."

A. Paulo Mwandishi wa Kitabu cha Wagalatia.

1. Mwandishi aliye mwanadamu ni Paulo mtume; mwandishi hasa ni Roho Mtakatifu.
2. Paulo: mtume wa Yesu Kristo na Mungu, 1:1; 5:2.
3. Mtume: aliyetumwa, mjumbe, balozi, 2 Wakor. 5:20; Waef. 6:20.
4. Sifa ya mtume ilikuwa kumwona Yesu, Mdo. 1:21-22. Paulo alimwona Yesu, 1 Wakor. 9:1; na aliitwa Naye, 1 Wakor. 15:8-9.

B. Mwisho Wake wa Kitabu: Makanisa ya Galatia.

1. Hasa katika sehemu ya kusini ya jimbo hili, makanisa ya safari za Paulo.
2. Safari ya kwanza ya Paulo: Selukia, Kupro, Salami, Pafo, Antiokia, Ikonia, Listra, Derbe, Mdo. 13:14. Wazee walichaguliwa, Mdo. 14:23.
3. Safari ya pili: aliwatembelea, "kila mji," Mdo. 15:36.

C. Sababu ya Maandiko: Waalimu Waongo Wenye Kuigeuza Injili.

1. Sababu ya maandiko imeonyeshwa wazi: wenye kuigeuza injili walikuja miongoni mwao, Wagal. 1:6-10.
2. Injili aliyoihubiri Paulo ni ile ambayo ilikuwa katika nia ya Mungu na kutimizwa ndani ya Kristo, War. 1:1-4, unabii ulitimia.
3. Alikuwa ni Yesu Kristo aliyesulibishwa, kwa ajili ya) dhambi, Wagal. 3:1; 1 Wakor. 15:1-4, uweza wa Mungu uletao wokovu, War. 1:16-17.
4. Kasoro ni injili "iliyogeuzwa" kwani hakuna injili nyingine. Anayeigeuza amelaaniwa na Mungu, 1:6-10.
5. "Injili iliyo tofauti."
    a. "Inaloga" - inaleta chini ya nguvu ya uovu, 3:1. Kile ambacho ni cha kushtusha au huba au ushirikina kinyume cha kweli ndilo jambo hili.
    b. Kutafuta "kukamilika katika mwili": kutoka kwenye roho hadi kwenye mwili, 3:3; Wakol. 1:20-23.
    c. Huadhimisha siku, nguvu ya mapokeo, 4:10; Wakol. 1:16-17

d. Wanaambatanisha na torati: "Tohara, na mapokeo yake, kumnyang'anya mtu uhuru wa injili, 5:2, 3, 6.

D. Mhutasari wa Jumla na Madhumuni ya Kitabu.

1. Binafsi: Utume wa Paulo, sura 1-2.
2. Fundisho: Torati na injili, sura 3-4.
3. Usihi: Kuushikilia uhuru wao, kuwa waaminifu, sura 5-6.

Mwisho: Ugomvi wa kale kati ya mapokeo na kweli, kati ya injili iliyogeuzwa, kati ya ulimwengu na dini la uongo na uEmwengu upande mmoja na Kristo na waaminifu upande mwingine unaendelea leo kama hapo kwanza. Somo liko sawa: Tii na kuishikilia injili, na usinaswe tena katika nira ya utumwa.

**INJILI ILIYOFUNULIWA**

Wagal. 1:11-22.

Azimio: Injili hiyo moja ni injili iliyofunuliwa kwa uwezo wa ishara wa Mungu mwenye enzi.

Shabaha: Kuonyesha ufunuo wa injili iliyofunuliwa.

Dibaji: Injili ya Yesu Kristo ni injili moja. Paulo anasema kuwa hakuna injili nyingine na yo yote iliyo tofauti na ile aliyoihubiri yeye mwenyewe ni injili iliyogeuzwa na yule anayeihubiri ananing'inia chini ya laana ya Mungu, 1:6-10.

Kisha injili aliyoihubiri na ambayo haina nyingine kando yake, imefunuliwa, haikugunduliwa.

A. Injili ya Paulo: Ufunuo Tukufu, 1:11-12.

1. Injili haikuwa ya kibinadamu katika hali yake si ya kibinadamu.
    a. Haikuundwa kufuata misingi ya hekima ya kibinadamu, 1 Wakor. 1:18-25.
    b. Haibadili-badiliki, inafaa kwa vizazi vyote, Waebr. 13:7; 13:8, 20.
2. Haikuwa na mwanzo wa kibinadamu. Wala Paulo hakuipokea kutoka kwa mwanadamu, wala hakufundishwa na mwanadamu, wala mitume au wafuasi wao. Haigunduliwi na mwanadamu, 1 Wakor. 2:7-9.
3. Lakini ilikuja kwa njia ya ufunuo:
    a. Vizazi vingine ambavyo havikujulikana, sasa vimejulishwa kwa njia ya Roho Mtakatifu, Waef. 3:4-5.
    b. Si kwamba Roho alifunua tu, bali alichagua maneno yale jinsi yalivyonenwa, 1 Wakor. 2:10-13.
4. Maisha ya awali ya Paulo hayakumpa maneno, 1:13-15. Mungu alichagua.

B. Injili ya Paulo: Wala Haikutolewa ns Mwili na Damu, 1:16.

1. Baada ya Kristo kujidhihirisha kwake, Paulo hakusemezana na ye yote. Huenda alisemezana na:
2. Gamalieli, mwalimu wake wa kale. Huenda Gamalieli alinena, Mdo. 5:39.
3. Baraza la Watu Sabini, baraza lililokuwa la juu zaidi baina yao. Hukumu yao huenda ilikuwa ya kupinga na kulaumu kwa kuwa walikuwa wenye ujuzi wa mambo ya Mungu.
4. Mafarisayo, wenye mapokeo: "Kurudia katika mapokeo ya mababu." Madhehebu wa siku hizi waWeza kutoa shauri kama hilo.
5. Masadukayo, wenye mambo ya mwili. Hawa huenda walicheka nia ya kwamba Kristo alimtokea, Kwani hao hawaamini katika Roho na uzima baada ya kifo.
6. Mama yake na baba yake, huenda walisema, "tungependa kukuona umekufa badala ya kwenda na kufuata kikundi hicho."
7. Rafiki zake vijana, wangesema, Paulo uyachukue mambo kwa uzito mno."
8. Lakini Paulo aliyakataa yote kwani alijua kuwa alilolisikia lilitoka kwa Bwana! 1:15-19.

C. InjiIi ya Paulo: "Mbele za Mungu Sisemi Uongo," 1:20.

1. Paulo alitambua kuwa atatoa hesabu kwa Mungu, na kwamba Mungu anatambua anaposemea, War. 14:12.
2. Mambo anayoandika kuhusu nalsi yake "ni ya kweli," 1: 20. Sura 1-2.
3. Mambo anayoandika kuhusu torati na injili "ni ya kweli," sura 3-4.
4. Kusihi na mazoezi "ni ya kweli," sura 5-6.

Mwisho: Namna yenyewe jinsi injili ilivyo huiondoa katika magunduzi ya kibinadamu na kuitangaza kuwa imefunuliwa.

Ushuhuda wa Paulo mwenyewe, akimwita Mungu ili ashuhudie, kunakazia kuvuviwa kwake na kwamba ilitoka kwa Mungu.

Nguvu yake yenyewekatika mioyo ya hao wanaoihubiri ila kuitii inaonyesha nakuhakikisha kuwa ilitoka kwa Mungu.

Mungu anakuita kwamba uiamini, uitii, na anakuahidia baraka zake. Je, utafanya hivyo wakati huu?

## INJILI MOJA ILIYOFUNULIWA IMEJARIBIWA

Wagal. 2:1-21.

Azimio: Iko injili moja tu kwa wote wawili Myahudi na Mtaifa.

Shabaha: Kuonyesha kwamba kuna injili moja tu, ukiwa wewe ni Myahudi au Mtaifa. wokovu huja kwa njia iliyo sawa sawa.

Dibaji: Katika sura ya kwanza ya Wagalatia tulijifunza kuwa kuna ile injili moja tu, 1:6-10. Ilionyeshwa pia kuwa injili hiyo ilikuwa na ufunuo tukufu, 1: 11-12. Katika sura ya pili tunaona injiIi hiyo moja ikijaribiwa. Ilijaribiwa pale Antiokia. Je, itakuwa ni injili moja kwa Myahudi na Mtaifa au mbili? Moja kwa ki1a mmoja? Au kukubaliana na rnafundisho ya Kiyahudi, arnbayo haitakuwa l1i injili, isipokuwa iliyo tofauti, injili iliyogeuzwa.

A. Matokeo ya Sura ya pili, 2:1-10.

1. Kuitembelea Yerusalemu: Paulo na Barnaba wametumwa na kanisa, lakini kwa ufunuo, Mdo. 15:1-3; Wagal. 2:1.
2. Paulo hakuuliza alilolihubiri, isije uradhi wake na safari yake vikawa bure, aIikutana na mitume kwa faragha, Mst.2.
3. Swala la Tito na Timothea na tohara, Mst. 3-5; Mdo. 16: 3. Paulo hajipingi mwenyewe. Timotheo alitahiriwa kuonyesha kabila lake kwamba alikuwa wa mbari ya Ibrahimu, Y oh. 7:22, na haikufanyika kwa kuonyesha kuitunza tohara kama sehemu ya torati. Hata hivyo, wazi kabisa wale waliataka kumtahiri Tito walitaka kumweka chini ya torati, kwa hiyo Paulo alikataa! Soma, Wagal. 5:2-4.
4. Kujitegemea kwake Paulo baina ya wale thenashara, na usawa wake nao kama mtume. Petro hakuwa na cheo zaidi kuliko Paulo - unaonaje kama mtu akimkemea Papa siku hizi! Iko injili moja ila kuna sehemu mbjlj pa kufanya kazi nayo, 2:6-10.

B. Swali Limepelekwa Yerusalemu Halikuchelewa Kumalizwa Kuliko Kulijaribu, 2:11-13.

1. Petro alikuja Antiokia," alikula na Mataifa, akikubali kuwa sheria ya Walawi haikuwa n nguvu. Petro alitumia unafiki, akitiwa nguvu na wengine waliotoka kwa Yakobo, Mst. 11-12.
2. Udhuru wa dhambi yake: maoni yake na kuhubiri kwake kwa Kornelio, Mdo. 10, hasa Mst. 34-35. Kwa hiyo, tabia yake, kama inavyoelezwa na Paulo, haikutokana na dhamiri yake, mwenyewe Petro, kwa hiyo, alitenda dhambi, War. 14: 23. Tabia yake katika mkutano kule Yerusalemu inahakikisha jambo hili zaidi ya kivuli cha mashaka, Mdo. 15:7-11.
3. "Wayahudi," Wakristo Wa Kiyahudi, pia walikuwa na ufahamu zaidi, lakini waliendelea vivyo hivyo na dhambi hiyo.
4. "Barnaba," bila shaka hili lilikuwa pigo kubwa kwa Paulo, "hata na Barnaba pia akachukuliwa," Mst. 13.
5. Barnaba alimtambulisha Paulo kwenye kanisa la Yerusalemu, Mdo. 9: 26-27. “Alikwenda" Tarso kumleta Paulo Antiokia, Mdo. 11: 25; kisha alisafiri .oa Paulo

kwa miaka minne, Mdo. 13-15: alisimama kando ya Paulo katika Antiokia na Yerusalemu, Mdo. 15: 1-3. Lakini sasa ameanguka, alitumia unafiki!
6. Kanisa - shida hii iliweka kanisa katika uchaguzi wa matatizo: Kukataa kuikubali torati na kuligawa kanisa au kuitikia na kuelekea, ambalo Utakuwa mbaya zaidi katika usafi wa injili.

C. Paulo, Shujaa wa Imani ya Injili, 2:14-21.
1. Katika upeo, Mungu alikuwa nashujaa wa Kweli Yake. Paulo alimkemea Petro mbele za wote, hadharani, Mst. 14. Ndivyo inavyotakiwa kuwa, 1 Tim. 5:20-2l.
2. Petro alikula na Mataifa, kwa njia hiyb akitangaza ubatili wa torati, sasa alikataa akitangaza kuwa ina nguvu, akijifanya mwasi, Mst. 17-18.
3. Katika injili Paulo alisulibishwa kutokana na torati na mambo yote yaliyohusiana naye, 2:20; Wakol. 2:14.

Mwisho: Hapa swali limemalizwa: Miongoni mwa mitume hamkuwa ukubwa, kwa hiyo, Petro hakuweza kuwa Papa! Miongoni mwa Wayahudi na Mataifa, hamkuwa na tofauti, kwa hiyo, injili moja kwa wote! Torati imeondolewa, injili moja tu imefunuliwa.

**KUSULIBIWA PAMOJA NA KRISTO**
Wagal. 2:20

Azimio: Mtoto wa Mungu lazima asulibishwe pamoja na Kristo, lazima ayafie mazoezi ya dbambi.

Shabaha:

1. Kuonyesha maumivu yenye mateso mno ya kuangikwa pamoja na Kristo.
2. Kuwasukumiza na kuwashawishi wasikilizaji wakitake kito cha aina hii.

Dibaji: Mtoto wa Mungu lazima ashiriki kuangikwa kwa Kristo kwa kusulibiwa kwa dhambi. Kifo kwa kuangikwo. ni kifo cha kutisha. Hata hivyo Paulo alitumia mfano akionyesha kuifia dhambi kwetu. Dalili ni mtano wenye nguvu wa kifo chenye kuumiza. Kuachiliwa kwetu kutokana na kukamatwa na dhambi mara nyingi kumetimizwa kwa juhudi na mo.umivu kwa upande wetu. Tanguo la dhambi ni njia yenye kuumiza.

Msemo huu umependezwa sana na Paulo, Wagal. 2:20; 5:24; 6:14; War. 6:8 Wakol. 2:20.

A. "Nimesulibiwa Pamoja na Kristo," 2:20.

1. Kuifia dhambi kwetu ndio sharti yetu ili tuishi na Kristo.
    a. Dhambi ni msimamizi wa kazi mkali na mkatili, Yoh. 8:34; War. 6:15-16.
    b. Utu wa kale wa dhambi lazima asulibishwe, War. 6:6.
    c. Ni usulibisho pamoja na Kristo, War. 6:6; Wagal. 2:20. Mapigano haya na dhambi yaweza kuwa kitu cha kuogofya kukiona, Waebr. 5:7-9.
2. Kwetu ni kifo pamoja na Kristo, kwani Yeye pia alipigana kuizuia dhambi isimfunikize, Waebr. 4:14-16; 2:9-10. Majaribu yake yalikuwa makubwa, Math. 4:1-10. Huzuni yake ilikuwa ya kutisha, Lk. 27:39-46.
3. UsuIibisho wetu ndiyo vita kubwa tutakayo pigana, angalia, Lk. 14:24; Math. 7:13-14; Wakol. 3:5-10 n.k. Ni vita, Wagal. 5: 16-17. Ushindi si mwepesi!

B. "Wala Si Mimi Tena Bali Kristo Yu Hai Ndani Yangu," Wagal. 2:20.

1. "Siishi tena," nafsi, dhambi na kuridhika lazima vife!
    a. Nafsi na dhambi lazima vitiishwe katika nia na mapenzi ya Mungu, War. 7:11; 7:14-16; 7:18-19; 7:10-24.
    b. Kristo anaweza na atawaokoa hao wanaomhuzunikia Yeye, War. 7:25; 1 Wakor. 15:55-58.
2. "Kristo yu hai ndani yangu."
    a. Nia yake lazima initawale mimi, Wafil. 2:5-8.
    b. Maisha yake lazima yaniongoze, Math. 20: 28; Lk. 19: 10.
    c. Tumaini lake lazima linitie nguvu, Y oh. 14: 13; 2 Wakor. 4:16; 5:1.
3. "Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani."
    a. Lazima niwe na imani inayohiari, Wafil. 4:13; Waef. 3:20-2l.
    b. Lazima niwe na imani inayopenda, 2 Wakor. 5:14.
    c. Lazima niwe na imani inayovumilia, Waebr. 11:27; Waebr. 10:39.

Mwisho: Usulibisho wa nafsi na mapigano yanayoendelea, kuona maumivu, lakini huzaa matunda yake ya amani, tunda la haki. Wewe unangojea nini?

**ROHO MTAKATIFU - KWA NJIA YA IMANI AU TORATI**
Wagal. 3:1-9.

Azimio: Roho Mtakatifu, ambaye ndiye uhakikisho wa kuhesabia haki kwa njia ya imani, alikuja kwa njia ya injili.

Shabaha : Kuonyesha jinsi Wagalatia walivyompokea Roho Mtakatifu kwa kuisikia imani.

Dibaji: Paulo alijitetea katika utume wake na maneno yake katika sura ya kwanza na ya pili; sasa anakuja katika kushikilia haki hasa kwa msemo au swali la kitabu: Je, watu huwekwa wenye haki mbele ya Mungu - kuhesabiwa haki - kwa matendo ya sheria au kwa njia ya imani ya Kristo?

Hoja ya kwanza: jaribio 1a ujuzi. Je, Walimpokea Roha kwa njia ya matendo ya sheria. au kwa kuisikia kunakotokana na imani?

A. Amri ya Paulo: Walilogwa na Jicho Ovu, 3:1.
1. "Nani aliyewaloga," akiwaleteni chini ya mvuto Wa "jicho ovu?" Mst. 1.
2. "Yesu Kristo a1iwekwa wazi mbele yenu kuwa amesulibiwa," aliwekwa kama tangazo 1a hadharani, kama katika Mdo. 13:2; 13:27; 13:34, 38; 14:1.
3. "Mnamwacha upesi, kwenda katika injili iliyo tofauti," 1:6-9.

B. Hoja ya Pili: Roho Mtakatifu kwa Njia ya Sheria au Imani, 3:2-5.
1. Roho Mtakatifu:
   a. "Je, mlimpokea Roho kwa matendo ya sheria, au kwa kusikia kunakatokana na imani," Mst. 2.
   b. Miujiza kwa njia ya imani au kwa njia ya matendo ya sheria," Mst. 5.
   c. Mtume anazungumzia nini Kukaa kwa Roho Mtakatjfu, au karama za miujiza za Roho, kipi? Vyote viwili ni sehemu ya mpango wa Mungu - Tafadhali angalia kwa makini:
   d. Roho Mtakatifu ameahidiwa kwa wote wanaotii injili, Mdo. 2:38; 5:32. Kama mtu hana Roho si wa Kristo, War; 8: 9-11. Mj,ili yetu ni hekalu za Roho, 1 Wakor. 6: 19-20; 3: 16-17.
   e. Kulikuwa na kupewa rasmi kwa Roho Mtakatifu katika kanisa la awali, Mst. 5. Lakini nguvu hii ya miujiza ilikuja TU kwa njia ya kuwekewa mikana ya mitume, Mdo. 8: 14-19; War. 1: 11; kama vile mitume wame-kwisha kufa na wale waliowawekea mikono juu yao, basi, karama za miujiza za Roho zimekoma, kama Paulo alivyosema kuwa itakoma, 1 Wakor. 13:8-10.
   f. Na vyote hivi ni kwa njia ya injili, na si kwa sheria.
2. Ukamilifu:
   a. "Baada ya kuanza katika Roho, mnataka kukamilishwa sasa katika mwili," Mst. 3. Je, Mungu anaugeuza mpango?
   b. Kwanza walikuwa katika mwili, War. 8:9; Wafil. 3:3-4.
3. Mateso:

a. "Mmepatikana na mateso makubwa namna hii bure?"
Mst. 4. Mambo waliyoteswa nayo walipomtii Kristo. Jinsi mateso yalivyokuwa hayajatajwa, lakini walionywa, Mdo. 14: 22.
b. Msalaba ulikuwa ni kikwazo. Wayahudi walimhcukia Paulo kwa kuwaleta Mataifa wasiotahiriwa katika kanisa bila tohara. Wote wangekubaliana juu ya jambo hili basi wasingewaudhi, kwa hiyo hili lilikuwa msalaba wa Krista, ukisimamia uhuru katika Kristo, 5:1.

A. Hoja ya Pili ya Paulo: Ibrahimu Alihesabiwa Haki kwa Njia Ya Imani, Si kwa Matendo ya Sheria, 3:6-7.

1. "lbrahimu alimwamini Mungu," Mst. 6. lmani ya Ibrahimu ilikuwa imani ya matendo, iliyofanya kazi, Yak. 2: 22-24.
2. "Wale walio wa imani, hao ndio wana wa Ibrahimu," Mst. 7. Hawa nao pia lazima wawe na imani ya matendo, inayofanya kazi ili wawe "wana wa Mungu," "wana wa Ibrahimu," Waga1. 3:26-29.
3. "Na kama wana wamepcwa Roho Mtakatifu," 4:4-7; kwa hiyo, kurudia sheria ni kupoteza vyote hivi.

Mwisho: Hakuna udhuru kwa ye yote kuongozwa kurudia katika utumwa ukiwa wa mafundisho ya Kiyahudi, ugeuzo wa sheria, au utumwa wa mambo ya Kimusa.
Kwa hiyo hakuna sababu au udhuru kwa ye yote leo kuongozwa katika utumwa wa makosa. Ndani ya Kristo mna uhuru. Anawakaribisha wote kuja kwake na kupata kupumzika na uhuru kutokana na dhambi, makosa na mambo ya kibinadamu. Je, utakuja?

## AHADI - SHERIA - NA INJILI

Wagal. 3:8-29

Azimio: Ahadi za Mungu kwa Ibrahimu, sheria ya Musa, vyote vimetimilika katika injili ya Yesu Kristo.

Shabaha: Kuonyesha naoma ahadi, sheria na injili vinavyotimilika ndani ya Kristo.

Dibaji: Juhudi ya kubandika sheria juu ya injili imekuwa wajibu kwa fujo za mwanadamu katika dini tangu siku ya Pentekosti. Pia bado kunafanya fujo hiyo hiyo leo.

Mungu ametimiza kila ahadi kwa Ibrahimu, na kuikamilisha sheria ya Musa ndani ya Yesu Kristo. Injili ndiyo mwisho wa ahadi na sheria, hatuingojei nyingine yoyote.

A. Ahadi iliyo ya Sehemu Mbili Iliyofanyika kwa Ibrahimu, 3:8-16.

1. "Ahadi aliyoifanya Mungu kwa lbrahimu," Mst. 8, Mwa. 2: 1·3; ilikuwa katika sehemu mbili: Kitaifa au nchi, 12: 1-7; na Kiroho, Mst. 3; Mwa. 22: 18; Ahadi ya kitaifa na nehi ilikamilishwa na agano, Mwa. 15: 18; na tohara, Mwa. 17: 1-13; "MwiIi" Mst. 13.
2. Ahadi ya Kitaifa ilitimilika wakati Israeli, chini ya Yoshua, walipoipata nchi, Yosh. 21: 43-45. Na ya kiroho ilitimizwa ndani ya Yesu Kristo, uzao, Wagal. 3: 8; 3: 16-17. 3. Hakuna mwandishi wa Agano Jipya aliyeunganisha ahadi ya Agano Jipya au fundisho na ahadi ya taifa au nehi, ila kila siku na ahadi ya kiroho. Kwa hiyo, hakuna ahadi ya nchi itakayotimizwa bado Yesu ajapo. Hakuna Wayahudi watakaorudia Yerusalemu wala Kristo hataanzisha ufalme wa kiulimwengu!

B. Sheria ya Musa na Ahadi ya Ibrahimu.

1. Kama urithi ni wa ahadi, vipi basi kuhusu sheria? Wagal. 3:18-19.
2. Sheria ya kitaifa, walipewa Wayahudi tu, Kut. 20:1-2; 34:27-28; 24:7-8; Kumb. 5:2-3.
3. Kwa watu rasmi, Wayahudi; kwa sababu maalum, kuwa ongoza mpaka wakati fulani, mapaka Kristo alipokuja, Wagal. 3:19.
4. Ni mambo mangapi ya Agano la Kale ambayo waandishi wa Agano Jipya wanayajumlisha katika neno "Sheria?" Mwanzo, Wagal.4:21; Zaburi, Yoh. 10:34; Manabii, 1 Wakor. 14:21; kuongeza na sheria yenyewe.
5. Vitu vitatu kutokana na sheria vinawavuruga watu leo: Sabato, lakini imekomeshwa, Wakol. 2: 14-16. Muziki wa vinanda kutoka katika Zaburi, lakini imekomeshwa, Yoh. 15:25; Ushirika wa wachanga kutokana na "tohara" katika mwili, sasa ni tofauti, Yer. 31:31.

C. Kukomeshwa kwa Sheria Kumebashiriwa.

1. Katikati ya Sinai na Msalaba, Yeremia alitangaza kupita kwa sheria ya kale Yer. 3:3. Mpya: Tofauti katika roho, mtu afundishwe kabla hajawa sehemu yake, dhambi hufutwa.

2. Sheria ya kale iliondolewa na Krista, msalabani, Math. 5:17-18; Yoh.19:28-30; Waef. 2:14-16; Wakol. 2:14-16.

IV. Sheria Mpya Imewekwa.

1. Mpya sasa imo kazini, Waebr. 8:6; 9:15; 10:9-10; Math. 26:28; Waebr. 13:20. Ya pili haikuweza kuwekwa mpaka ya kwanza ilipoondolewa.
2. Mamlaka yote sasa ni yake Kristo, Math. 28:18-20; kwa hiyo hakuna mamlaka katika sheria ya kale. Kristo anayo mamlaka yote ambayo Musa hakuwa nayo!
3. Mataifa yote yanajumlishwa: Wafundishwe kuamini, kutubu, na kubatizwa, Mk. 16: 15-16; Lk. 24: 46-49; Tohara ni moyoni, War. 2: 28-29; Wakol. 2: 11-12.
4. Ubaguzi wote wa kikabila, kitaifa vyote vimekomeshwa; wote wamekuwa wapya, Wagal. 3:23-29; 2 Wakor. 5:17.

Mwisho: Yesu Kristo anaitimiza ahadi ya Kiroho: Baraka zote za Mungu sasa zimo ndani yake. Waliomo ndani yake ni watoto wa Mungu kwa njia ya imani, wana wa Ibrahimu na warithi wa ahadi. Hili Kristo anakukaribisha kuja na kujumlishwa katika yote ambayo Mungu anayo kwa ajili ya kila mtu.

**FUMBO LA SARA NA HAJIRI**
Wagal. 2:21-31

Azimio: Agano la sheria limetupwa, kwa hiyo, hatupo chini ya sheria.

Shabaha: Kuonyesha jinsi Paulo anavyolinganisha maagano mawili, mojawapo ambalo ni la kimwili kwa hiyo, limeondolewa, ha ambapo lingine ni la kiroho ambalo lingalipo.

Dibaji: Mtume ametoa hoja kuhusu shabaha ya wokovu kwa njia ya imani ndani ya Kristo kinyume cha wokovu kwa njia ya matendo ya sheria; pia na Ahadi na sheria. Hoja hizi tena zitafanyika: Vana na kawaida za kwanza za dunia, tabia yao wakati Paulo alipokuja kwao mara ya kwanza, na kutokana na fumbo la wan awake wawili. Tutanadharia tu cha kwanza na cha mwisho katika kisamo hiki.

A. Uana Na Uhuru Kushindana Na Kawaida Za Kwanza Za Dunia Na Utumwa.

1. "Nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani," 3:23-29; "Maana ninyi nyote mlibatizwa katika Kristo," (hii ndiyo njia pekee inayofundishwa na Agano Jipya jinsj anayeamini anavyoweza kuingia ndani ya Kristo). Kwa hiyo, u mzao wa Ibrahimu, warithi wa ahadi.
2. Wayahudi, kabla ya kufikia utu uzima, 3:23; 4:1-2, walikuwa katika hali ya utumwa katika kawaida za kwanza za dunia, "mambo ya kuadhimisha" ya sheria, 4: 1-3. Lakini sa sa wako huru, kwa umri, katika Kristo, 4:4-7; "Utimilifu wa wakati," Mk. 1:14-15; Mdo. 3:24-25.
3. Mataifa, kabla Kristo hajaja, walikuwa utumwani kwao sio miungu vile vile na utumwa katika mambo ya unyonge, 4:8-9.
4. "Kwanini kurejea tena mafundisho ya kwanza yaliyo manyonge, yenye upungufu, ambayo wanataka kuyatumikia tena?" Mst. 9-10. Ikiwa ni Myahudi au Mtaifa wakirudi katika njia zao za kale au wote katika mafundisho ya Kiyahudi basi waIikuwa nj wa sheria, Mst. 21.
5. Kushika siku kuu za dini kumekatazwa na Mungu, Mist. 10-11. Dini zote za uongo zinafanya jambo hili hili!

B. Hoja Kutokana na Fumbo la Sara na Hajiri, 4:21-31.

1. "Ninyi mnaotaka kuwa chini ya sheria," 4: 21. Namna Agano Jipya inavyotumia neno "sheria" Jinajumlisha na Mwanzo pia, Wagal. 4:22; Kutoka, War. 7:7; Walawi na Kumbukumbu La Torati, katika Matt. 22:35·37. Hesabu, Math. 12: 5; Zaburi, Yoh. 10: 34; Manabii, 1 Wakor. 14:21; katika msemo mwingine Agano La Kale lizima.
2. Fumbo:
    a. Wanawake wawili wanasimamia maagano mawili, 4:22-27.
    b. Wana wawili: Watu wawili: kimwi.li na kiroho; mmoja katika utumwa mmoja huru. lbrahimu alimwondoa mwanamke wa utumwa pamoja na mwanawe, 4:28-30.
    c. Visomo: Agano la sheria limeondolewa, hatupo chini ya sheria (kwa hiyo wa Seventh-Day Adventist wanaoitunza Sabato wanakosea!) Israeli wa kimwili ameondolewa, hatarithi pamoja na aliye huru. (Kwa hiyo

wenye Utawala wa miaka EUu wamekosea, wanaofundisha Ufalme wa Kidunia kwa ajili ya Wayahudi!) Ikiwa Israeli wa mwili anarithi na mwingine hawezi; ikiwa wa kiroho anarithi, basi wa kimwili hawezi! Kwa hiya hakuna "Utawala wa miaka elfu pande zote!

3. "Ndiposa, ndugu zangu, sisi si watoto wa mjakazi, bali tu watoto wa huyo aliye mwungwana." 4: 31.

Mwisho: Kanisa na lipiganie lea kujiweka safi na injili iwe huru kutokana na sheria za utumwa. Huru mbali na mapokeo, huru mbaIi na siku kuu katika dini, kama vile Pasaka, Kristmasi n.k. kwani hivya ni vya sheria.

**UHURU KATIKA KRISTO**
Wagal. 5:1-15

Azimio: Kristo ameshamweka mkristo kuwa huru, kwa hiyo, lazima asimame imara na asiletwe chini ya kongwa la utumwa tena.

Shabaha: Kuonyesha uhuru wetu ndani ya Krista na kuitikia onyo la kusimama imara.

Dibaji: Watu huzungumzia "uhuru" na "kuufia uhuru" na "uhuru wa kisiasa." Lakini kuna uhuru aina moja tu hasa: uhuru kutokana na dhambi na makosa ya wanadamu. Yesu alikufa kuwaweka watu huru. Sisi kama wakristo lazima "tusimame imara" katika uhuru huu na kupinga kila jaribio la kutufanya watumwa tena.

A. Uhuru wa Mkristo Ndani ya Kristo, 5:1.

1. Kristo alipokuja ulimwengu wote ulikuwa katika utumwa kwa yule mwovu, 1 Yoh. 5:18; War. 3: 8-10, 23.
2. Wayahudi walikuwa katika utumwa kwa dhambi, Yoh. 8:32-36.
3. Mataifa walikuwa katika utumwa kwa miungu ya washenzi, Wagal. 4:8.
4. Wate wawili walifanywa huru kutokana na mambo yote kwa ambayo wasingefanywa huru kwa nafsi zao wenyewe, kwani sasa ni wapya katika Kristo, Wagal. 3:26-27; 2 Wakor. 5:17. Basi iwe ni imara!

B. "Msinaswe Tena Chini ya Kongwa 1a Utumwa," 5:1.

1. Hatari Wakati Ule:
    a. Mafundisho ya Kiyahudi yaliweka tisho kwa wakristo Wagalatia, 5:1-12.
    b. Filosofta iliwatisha wakristo wengine mahali pengine, Wakol. 2:8-10.
    c. Mapokeo ya wanadamu yalitisha, Wakol. 2:8.
    d. Ulimwengu uliviona hivi, Wagal. 5:13-15.
2. Hatari Leo:
    a. Mafundisho ya Kiyahudi yanalitisha kanisa kutoa cha kumi, muziki wa vinanda, kutunza Sabato na Utawala wa Miaka Elfu!
    b. Filosofia bado inaleta kichwa chake kibaya, mambo ya kisasa, kukana kuwa Biblia si neno la Mungu lililovuviwa; kukua, vyote ni filosofia ya kibinadamu.
    c. Mapokeo; ubatizo wa wachanga; utawala wa kanisa uHoharibiwa; Petro kama Papa, vyote kutokana na wanadamu, si Mungu! Angalia! Simama Imara Ndani ya Kristo!

C. Uhuru Katika Kristo Si Hati ya Kufanya Dhambi, 5:13-15.

1. "Msiutumie uhuru wenu kwa ajili ya dhambi," 5:13.
2. "Tumikianeni," Wagal. 6:1-2.
3. "Umpende jirani yako kama nafsi yako," 5:14. Angalia tabia yako, War. 14:13-16.
4. "Angalieni msije mkaangamizwa." 5:15. Chuki yote na faraka viondoshwe, Wakol. 13:8-10.

Mwisho: Mungu hufurahi na kutukuzwa tunapotenda haki. Sheria haiongezi lolote katika ukamilifu wetu na utimilifu katika Kristo. Wala filosofia au mapokeo ya wanadamu wala ulimwengu haviwezi kumsaidia mkristo, ila tu vinatufanya watumwa na kutuleta chini ya kongwa la utumwa.

Wote waliomo katika utumwa lazima waje kwa Kristo ili wawekwe huru, kisha wasimame imara na kufurahia katika uhuru pekee wa ulimwengu mzima.

**MATENDO YA MWILI (1)**

Wagal. 5:16-21

Azimio: Wanaojizoeza katika matendo ya mwili hawataurithi ufalme wa Mungu.

Shabaha: Kuonyesha matendo ya mwiIi na kuwawezesha wakristo kuyaacha.

Dibaji: Katika Dfunuo sura ya kumi na nane "pana mae1ezo kuhusu kuanguka kwa Babeli. Nt tumaini langu kuwa Babeli inasimamia ulimwengu wote wenye kufanya mambo ya kjmwiJi, kwenye tamaa, kama mmoja wapo, wa maadui wa kanisa. Tamaa za mwili daima zimekuwa njia ambamo shetani anafanyia majaribu: Edeni, Mwa. 3:1-6; Yesu, Math. 4:1-10; Mkristo, 1 Yoh. 2:15-17; Paulo anaonyesha tamaa hizi, Wagal. 5. Katika somo hili tutaona tatu za tamaa hizo.

A. Nguvu Mblli Kubwa Zinazopingana Katika Viungo: Roho Na Mwili, 5:16-18.

1. "Hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili," Mst. 16. Hii ni hali yetu ya kimwiIi inayotamani kutenda dhambi na kuitumia miili yetu na nia kutumikia dhambi.

a. Utani mbaya, huleta picha ya maneno mabaya, Math. 12:34-37; 15:19-20; Waef. 5:3-5.

b. Mavazi yasiyofaa, ya uzinifu katika hali, 1 Tim. 2:9; Math. 5:20.

c. Kucheza dansi, kujinyonga-nyonga katika mwili, kukutana kwa via viwili tofauti, 1 Yoh. 2:15-17; Kuto. 32:26; 32:19; 1 Wakor. 10:7.

d. Kupapasana kwa vijana. Vyote vyaweza na mara nyingi huongoza katika moja au zote tatu hizo, dhambi za kutisha.

2. Mkristo amekwisha kuonywa kuhusu tabia hiyo, Waef. 5:7-12; kwa hiyo Mwangalie!

Mwisho: Dhambi hizi ni kinyume cha ma1sha ya Roho. Kuendelea katika dhambi hizi ni kupoteza maisha ya milele, lakini kuzifisha sasa ili kuishi milele hapo baadaye!

## MATENDO YA MWILI (2)

Wagal. 5:21-22

Azimio: Hao wanaojizoeza katika matendo ya mwili hawataurithi ufalme wa mbinguni.

Shabaha: Kuonyesha matendo ya mwili na kuwawezesha wakristo kuyaacha.

Dibaji: Kama kitu chaweza kumzuia mtu asipate furaha iliyo ya juu duniani, na kisha kumpc1eka jehanamu kwa milele hapo baadaye, basi anaye mwonya kuhusu jambo hili lazima afikiriwe kuwa ni rafiki sivyo? Wagal. 4:16.

A. Mwenye Dhambi Anaaftza Uhusiano Mpya kwa Mwenzi Wake na Hupata: Tabia Mpya Anapokuwa Mkristo.

1. "Katika ungwana huo Kristo alituandika huru," 5:1. Yesu alisema twaweza kuwa "huru katika kweli, Yoh. 8:32; 8:34. Huru mbali na utumwa wa dhambi na sheria, War. 6:1-2, 11; 6:15-16. Isitumike kama hatj kwa kutenda dhambi, Wagal. 5:13.

2. "Tumikianeni kwa upendo," Mst. 5:14-15. Kuna uhusiano mpya: na majirani, katika amani, War. 12:18; Waebr. 12:14; kanisa, katika umoja, Yoh. 17: 20-21; Waef. 4:1-3; 1 Wakor. 1:10.

B. Matendo ya Mwili - Dbambi Zinazobaribu Utaratibu wa Jamii Zinazobalifu Tabia na Uhusiano Mpya, 5:21-22.

1. "Uadui" Mst. 20, hali ya uhasama, roho ya uadui, hasa huonyesha chuki. Kinyume cha roho ya Kristo, Lk. 23:12; War. 8:7; Waef. 2:14-15. Huharibu mapendeleo ya jamii! Yoh. 4:9.

2. "Ugomvi" Mst. 20. Mafarakano yenye hasira, kupigana, kugombana, namna ya uadui; hivi ni vya mwili, 1 Wakor 3:3; huishia katika mauti ya roho, War. 8:6.

3. "Wivu," Mst. 20, ushindani wa wivu na faraka. Waweza kuwa kwa ajili ya cheo katika dini au fahari, hata hivyo ni ya kimwili, Yak. 1:19-20; 1 Tim. 2:8.

4. "Fitina," Mst. 20, chama katika chama, ushirika usio wa kawaida wa watu wanaopendelea, roho isiyodharau matendo ya chini ili kufikia mwisho wake, Yak. 3:14-16; Wafil. 2:3; War. 12:10.

5. "Faraka," Mst. 20, matengano, kutokubaliana, ndani ya kusanyiko, 1 Wakor. 1: 10-14; Wafil. 4:2-3.

6. "Uzushi," Mst. 20, vita vinavyotokana na hitilafu ya mawazo na lengo. Huwezi kumtenganisha mwalimu wa uongo na mafundisho yake, lazima kujitenga nao, War. 16:17-18; pia na wenye "fitina." .

7. "Husuda," Mst. 20, kujipenda au asiye na urafiki, mchoyo katika mambo aliyo nayo mwenzi wake. Kutokuwa na furaha kunakotokana na kufanikiwa kwa mwingine, Tit. 3:3; 1 Pet. 2:1.

C. Tokeo na Dawa ya Dbambi Hizi.

1. Tokeo: Watu hawana furaha; machafuko na matendo maovu katika kanisa na nyumbani; urafiki unavunjwa mioyo inahuzunika, makanisa yametengana. Mtu

anayejizoeza haya, na kusanyiko zinazo watetea hawa ni ya kuchukiza kwa Mungu na jamii!

2. Dawa: Tubuni! Tubuni au mtaangamia, Lk. 13:3; Wagal. 5:21; Ichimbueni Roho ya Kristo, Wagal. 5:14; 5:22; enendeni kwa roho katika maisha yenu.

Mwisho: Maisha haya karibuni yatapita na tutasimama katika hukumu mbele za Kristo; si waasherati tu, bali pia na hao wenye roho zilizo ovu wanaowachukia ndugu - ni wenye moyo safi tu ndio watamwona Mungu, Math. 5:8.

**MATENDO YA MWILI (3)**
Wagal. 5:22

Azimio: Hao wanaojizoeza katika mambo ya mwili hawataurithi utalme wa mbinguni.

Shabaha: Kuonyesha matendo ya mwili na kumwezesha mkristo kuyaacha.

Dibaji: Bila kujali jinsi gani tunajaribu kuahirisha uzee hatimaye huja. Mwili lazima uzeeke na mwishowe kuoza, 2 Wakor. 4:16; 5:1; Lakini kama mashine, matunzo safi yataendeleza miaka yake ya kufanya kazi. Waebr. 9:27; 2 Pet. 1:14.

A. Mwili wa Mkristo – Hekalu la Roho Mtakatifu.

1. Kuna miisho miwili ambako mkristo aweza kwenda:
Aweza kushibisha mwili wake kama ndio ulio bora zaidi, mwisho mwingine: Kuudharau kama ulikuwa ni ubatili. Mwili wa Mkristo na maskani ya Roho wa Bwana, 1 Wakor. 6: 12-20; Lazima uhifadhiwe katika utakatifu, War. 12:1-2; Kristo atukuzwe ndani yake, Wafil. 1:20; wakati huo huo mwili lazima kuutumikisha. 1 Wakol. 9: 27.

2. Mtu atahukumiwa kwa matendo aliyoyafanya katika mwili, 2 Wakor. 5:10. Sasa tunao mwili wa "aibu" kisha tutakuwa na mwili wenye utukufu, Wafil. 3:20-21; 1 Wakor. 15:42-44. Mwili usiwe ndicho kitu muhimu katika maisha, Lk. 12:22-23; au kuuangalia sana hata kupoteza maisha ya kiroho, Lk. 21:4. Lakini ufikiriwe kwa mambo ambayo Mungu aliutayarishia.

B. Matendo ya Mwili - Dhambi za Kuzidisha, 5:21.

1. "Ulevi," Mst. 21, kulewa, matokeo ya kuzidisha kunywa. Angalia! 1 Wakor. 5:11; 6:9-10; Kileo hufanya kazi mwishoni, Mith. 23: 29-33; matokeo ya kileo: luu ya ubongo, hukomaa, na chembechembe za damu hufa wala hazidili zingine tena, huharibu maini, moyo, mishipa huwasha, na tando 1a tumbo. Misuli huwa teketeke; husaidia kuharibu mawazo, wema hutcswa, akili hupungua. Watu huwa na hatia juu ya dhambi wazitendazo wangali wamelewa! Nyumba huharibiwa, matengano na talaka, watoto kudharauliwa, jamii huteswa, urafiki huvunjika, mwishowe roho hutengwa na Mungu na kupotea katika jehanum, Isa. 59:1-2. Mkristo au ache unywaji kabisa!

2. "Ulafi," Mst. 21, hasa katika karamu, kunywa kwa uchelewevu na lile linaloamsha mambo ya ashiki. Kushiriki mambo ya tamaa, na hata katika arusi au mikusanyiko ya aina hyo. Hii imelaumiwa.

3. “Na mambo yanayofanana na hayo," Mst. 21. Hizi ni dhambi zilizo za aina moja. ambazo ni za kimwili na ni kinyume cha roho wa Mungu. Mara nyingi hili litajumlisha madawa, tumbako, ulafi, ashiki na kadhaIika! Mkristo lazima ajiepushe na unajisi, 2 Wakor. 7:1. Kitu gani kinacho kuzuia? Basi kiondoe!

Mwisho: Matendo ya mwili hututenga na Mungu. Mkristo lazima auache ulimwengu na mambo yake ya kutamanisha ili aokolewe, 2 Wakor. 6:14-19. Mkristo na akumbuke kuwa mwili wake ni hekalu la Roho wa Mungu, Roho Mtakatifu, na kwa hiyo, na autumie mwili wake kwa utukufu wa Mungu.

**ROHO NA TUNDA LAKE**

Wagal. 5:16-17; 5:22

Azimio: Hao wanaojizoeza tunda la Roho watаurithi ufalme wa Mungu!

Shabaha: Kuonyesha jinsi lazima mkristo ausulibishe rnwili ili azae tunda la Roho.

Dibaji: Vita waliyopigana Wagalatia ilikuwa sawa na ile anayopigana kila mmoja leo. Kila mmoja lazima apambane na shida zile zile, kuushinda udhaifu ule ule, kushinda kwa Roho yule yule. Katika sarno hili tunataka tutazame mapigano ambayo ni ya kiIa mmoja wetu.

A. Mchezo Mkubwa wa Maisha - Mapigano ya Mwili na Roho, Wagal. 5:16-17.

1. "Nyote ni wana wa Mungu," 3:16-27. Waliitii injili na ni warithi wa ahadi, 3: 28-29.
2. "Mungu alimtuma Roho, miongoni mwetu," 4:6-7, kwa hiyo, tuwe na Roho wake.
3. "Enendeni kwa Roho," Wagal. 5:16-17. Tukitiishwa kwa Mungu, sasa enendeni hivyo!
4. "Kwa sababu mwili hutamani kushindanana Roho," 5:17. Katika kila mmoja mna mapigano yanayoendelea! Imezungumzwa katika War. 7:22-25.
5. "Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima imeniacha huru mbali na sheria ya dhambi na mauti," War. 8:1-2.
6. "Tumo katika Roho kama Roho wa Mungu anakaa ndani yetu," War. 8:9-11.
7. "Tu wadeni kwa Roho," War. 8:12-17. Mstari wa vita umechorwa wazi, ni mwili ukipigana na Roho!

B. Kusudio la Vita: Kuisulibisha Nafsi. 5:24.

1. "Hao walio wa Kristo Yesu ameusulibisha mwili," Wagal. 5:24.
2. "Nimesulibiwa pamoja na Krista," 2:20.
3. "Kristo yu ndani yangu," 2:20.
4. "Ulimwengu umesulibishwa kwangu," Wagal. 6:14.
5. “Tukizikwa pamoja naye, sasa tumefufuliwa,” Wakol. 2:11-13.
6. "Kutafuta mambo yaIiyo juu," Wakol. 3:1-4.
7. "Nautumikisha mwili wangu," I Wakor. 9:24-27.

C. Baada ya Kusulibiwa: Lazima Nizae Tunda la Roho, Wagal. 5:22.

1. "Yafisheni matendo ya mwili," Wakol. 3:5.
2. "Wameusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake," Wagal. 5:24.
3. "Kristo akae katika mioyo yenu kwa njia ya imani," Waef. 3:16-17.
4. "Lakini tunda la Roho," 5: 22. Maisha yetu sasa yanazaa tunda IiIilo tofauti. Tunda linalozaliwa kutokana na mizizi na kiwiliwili, kutoka kwa ndani - ndivyo lilivyo tunda la Roho. Ni matokeo ya upandaji wa Kristo kwa ndani.
5. "Tunda la Roho," 5:22. Likimaanisha Mungu:

a. "Upendo" Mungu ni upendo - 1 Yoh. 4:7; pasipo upendo, tu baridi, tumekufa, 1 Wakor. 13:1-3.
b. "Furaha" - Kristo ni furaha. Alikuwa "mtu wa huzuni" bali kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbe1e zake, Waebr. 12:2; aliyomwahidi mkristo, Yoh. l5:11.
c. "Amani" - katika Roho Mtakatifu utulivu wa moyo, Yoh. 14:27. Amani yake huwa yetu anapotawala Roho yetu, Wafi1. 4:4-7.

6. "Tunda la Roho," 5:22. Likimaanisha mwanadamu:
a. "Kuvumilia" - kama Kristo alivyodhihirisha uvumilivu wa Mungu kwetu, 2 Pet. 3:9.
b. "Huruma" - akiongozwa na Roho wa Kristo mkristo hawezi kuwa kitu kingine, Wakol. 3:12.
c. "Wema" - wema wetu lazima udhihirishwe kwa wengine kama nuru inavyoangaza, Math. 5:16.

7. "Tunda la Roho" 5:22. Likimaanisha nafsi:
a. "lmani" -- waaminifu. Mkristo lazima aitunze imani pamoja naye kila siku, War. 14:23.
b. "Upole" - uhiari wa kukubali mapenzi ya Mungu kirehema, kiIa siku, bila kujali nafasi au sababu, Math. 5:5; 1 Pet. 3:4; l Wathes. 2:7.
c. "Subira" - kushinda nafsi, lazima ajifunze na iwekwe katika mazoezi. Kuongoza matakwa ya mtu kwa maongozo ya Mungu katika neno, 2 Pet. 1:6; kinyume na dhambi za mwili na Roho aliye juu.

Mwisho: Sote tu sawa katika majaribu na udhaifu, na kuna njia moja tu ya ushindi: Kristo na Roho Wake ndani yetu, tukiongozwa na neno, tukijizoeza katika subira katika mambo yote, War. 13:14.

## KUREJEZA ANAYEPOTEA

Wagal. 6:1-5

Azimio: Maandiko yanafundisha kuwa Sisi ni wahifadhi wa ndugu yetu. Tumrejeze anayepotea.

Shabaha: Kuonyesha lini na namna hatuna budi kumrejeza mkristo anayepotea.

Dibaji: Paulo amezungumzia hatari mbili zinazolikabili kanisa: Mafundisho ya Kiyahudi na Mambo ya Ulimwengu. Sasa anakuja katika kazi iliyo kubwa hasa ya kuwarejeza ndugu wanaopotea. Mara nyingi mno baada ya mtu akisha ongoka na kisha akianguka inaonekana kwamba kunakuwa hakuna yoyote anayekuwa na wajibu wa kumrudisha.

Ziko aina mbili za tabia ambazo watu huonyesha juu ya mkristo anayepotea: Wengine ili wakali mno kama Mafarisayo. Hata hivyo dhambi ni dhambi tu, 1 Yoh. 3:3-4; War. 6:23; Yak. 1:13-15. Katika soma hili tunakusudia kufikiria tabia ya kiroho ya mkristo juu yake anayepotea.

A. "Mtu Akighafilika Katika Kosa Lo Lote Ninyi MIio Wa Roho Mrejezeni Mtu Kama Huyo kwa Roho ya Upole, UkijiangaJia Nafsi Yako Usije Ukajaribiwa Wewe Mwenyewe," 6:1.

1. "Mtu akighafilika," Mst. 1. Hii ni dhambi ya ghafula, si iliyopangwa. Lakini umeshikwa nayo pasipo tahadhari kama Petro, Math. 26:69-75. Si ya "kujitakia" kama ya Waebr. 10:26-31; ila kwa ajali tu.
2. "Ninyi mlio wa Roho," Mst. 1. Hao wanaoongozwa na Roho, 5:16, wakizaa tunda la Roho, 5:22-24.
3. "Mrejezeni upya mtu kama huyo," Mst. 1. Mmrejeze katika ushirika wa Kristo. Dhambi huvunja ushirikiano wetu na Mungu na Kristo, 1 Yoh. 1:3-7; Mmrejeze mtu huyo arudie katika nduguze.
4. "Kwa roho ya upole," Mst. 1. Hii ndiyo tabia ya walia wa roho, tunaonekana kwa huruma kwa wenye dhambi, 5:22-25; Wakol. 3:12-17; 1 Wathes. 5:12-13.
5. "Ukijiangalia nafs; yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe," Mst. 1. Kila siku ukumbuke kuwa unaweza kuanguka pia 1 Wakor. 10:2. Roho hii ni kinyume cha ile ya Kifarisayo, Lk. 18:9-12.

B. "Mchukuliane Mizigo na KlIitimiza Hivyo Sheria ya Kristo," 6:2.

1. "Mchukuliane mizigo," Mst. 2. Mzigo huu ni "mzigo ulio mzito mno" ambao anayepotea hawezi kuubeba peke yake. Hili linafanya kila mkristo kuwa mhifadhi wa ndugu yake, Mwa. 4: 9. Kila mmoja aweza kuwa na "mzigo mzito mno" anapoteleza katika dhambi, kwa hiyoinatubidi kupiga hatua na kumsaidia kuubeba "mzigo wake mzito." Haya ndiyo "mapenzi ya Kristo."
2. "Kuitimiza hivyo sheria ya Kristo," Mst. 2. "Sheria ya upendo, sheria ya Kristo," imo katika Yoh. 13:34-35 kwa muhtasari. Kama vile Kristo alivyotupcnda na kutuangalia kwa upole, vivyo nasi yatubidi kuwasaidia "wanaolemewa," Math. 12:20.

a. Wanawake kisimani, Yoh. 4.
b. Mwanamke aliyekamatwa katika uzinzi, Yoh. 8.
c. Mwivi msalabani, Lk. 23:43.

C. "Maana Kila Mtu Atalichukua Furusi Lake Mwenyewe," 6:5.

1. "Kila mtu alichukua furusi lake mwenyewe," Mst. 5. Kila mkristo aubebe mzigo wake mwenyewe, kama vile wote wanao mzigo wa kubeba. Na kama Kristo, tunao msalaba wa kubeba, Math. 16:21-24.
2. Kila mmoja aipime kazi yake mwenyewe, Wagal. 6:3-4. Kila mmoja atatoa hesabu yake mwenyewe Hukumuni, War. 14:1-12.

Mwisho: Hali ya kibinadamu ni ya unyonge mno. Kila mmoja atambue unyonge na mahitaji ya ndugu zake, na kwamba naye pia, anao unyonge katika hali yake. Tunapotaka kumwokoa ndugu anayepotea, tuwe wapole na wenye huruma kila siku tukiwa waangalifu kwamba Shetani hatunasi katika dhambi hiyo hiyo, kwa jaribu hilo hilo.

Na tusaidiane kuhimiza kila mmoja katika upendo na matendo merna, Waebr. 3:12-13; 10:24-25.

**KUPANDA NA KUVUNA**
**Mavuno Yetu Ya Kiroho**
Wagal. 6:6-9

Azimio: Lo lote tupandalo, ndilo tutakalovuna.

Shahaha: Kuonyesha sheria ya Mungu isiyobadilika kuhusu kupanda na kuvuna.

Dihaji: Mavuno yetu ya kiroho kutegemea .iuu ya pando letu la kirono. Kama njia zote za Mungu, mambo ya kiroho yanasimama juu ya sheria na si juu ya bahati. Katika tabia na roho, shangwe au furaha tunakuwa jinsi tunavyopanda. Kwa hiyo uangalic jinsi unavyopanda! Kwani mavuno hayaepukiki!

A. Kanuni ya Mungu Isiyobadilika:" Apandacho Mtu Ndicho Atakachovuna," Wagal. 6:7.

l. "Mungu nadhihakiwi," Mst. 7. Mungu hadanganyiki, kuchekwa, hakuwezi kuwa ndimi mbiH kwa Mungu, Waebr. 4:13. Tazama Ayu. 15:31; Yer. 37:9; Oba. 3; Lk. 21:8; 1 Wakor. J 5: 33. Huwezi kumdanganya Mungu!

2. "Cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna." Mst. 7. Mungu aliifanya amri hii hapo mwanzoni, Mwa. 8:22; Hos. 8:7. Wingi pia hutegemea juu ya upandaji kwa wingi, 2 Wakor. 9: 6-9. Wakristo wengine huwa hawapandi Lo Lote!

B. "Maana Yeye Apandaye Kwa Mwili Wake KatikaMwili Wake Atavuna Uharibifu," 6:8.

1. Taifa:
   a. Linayoyapanda taifa hayo 1itavuna! Kanuni ni ile ile!
   b. Dini na upotovu vyaweza kuangamiza taifa, Zab. 33:12; Mith. 14:34; Zab. 9:17; Oba. 3.
   c. Taifa linalopanda uharibifu, uchoyo, tamaa. kwa mwili litavuna kupungukiwa, ufukara, na huzuni. Kama taifa linapanda fidhuli, dharau ya mataifa mengine, kwa hiyo litavuna kuanguka. Jina ya zetu ni matokeo ya upandaji wetu mbaya, Hos. 8:7.
2. Kanisa:
   a. Kusanyiko lisichukuane na dhambi na mafundisho ya uongo, 1 Wakor. 5:13. Kufanya hivyo ni kupanda kwa mwili na 1itavuna uharibifu, 1 Yoh. 2:15-17.
   b. Kusanyiko lisipande kutojali, ulegevu, kufanya hivyo ni kuvuna upotovu, 1 Wakor. 5:6-7.
   c. Kusanyiko kila siku 1iwe macho kupinga magomvi, faraka, na mengineyo, 1 Wakor. 3:1-6; Yak. 3:16.
3. Jamii:
   a. Jamii ndio msingi wa taifa, kama haina nidhamu taifa litaanguka! Waef. 6:1-2. Tafadhali soma, 1 Sam. 3:10-14.
   b. Jamii lazima ionyeshe ukristo kama nuru inayong'aa, Math. 5:13-16.
   c. Jamii lazima iusimamie ukweli na wema, Math. 5:32.

4. Mtu Binafsi:
   a. Tangu ujana hadi uzee, kanuni ni ile ile, Mhu. 11:9-10; 12; 13.
   b. Dhambi yaweza kuongoza katika maangamizi tu, War. 6:23; Lk. 12:4-5.
   c. Wewe unapanda nini? Hasira? Uasherati? Ulevi? Kutamani? Au "matunda ya roho?"

C. "Apandaye Kwa Roho Katika Roho Atavuna Uzima Wa Milele," Waga1. 6:8.

1. "Apandaye kwa Roho," Mst. 8. Tunapanda katika Roho kwa kuyatii maneno ya Roho, Zab. 126:5-6; Mhu. 11:6; Isa. 32:20; Yak. 3:18.
2. "Atavuna uzima wa milele," Mst. 8. Hatutakuwa na furaha zaidi katika maisha haya tu bali tutapokea uzima wa milele baada ya kitambo kidogo, Math. 19:29; Lk. 18:30; Yoh. 4:14; 4:36; 6:27; War. 6:22; Yuda 21.
3. Tunda la Roho ni matokeo ya upandaji. Kila wazo, tendo, neno lazima litawaliwe na kutumwa kwa ajili ya Kristo na kanisa, Tukifanya basi dhamana tulivu ya Paulo itakuwa yetu, Wafil. 4:11-12; 2 Tim. 4:1-8.

D. Mwisho Halisi Wa Mavuno, Math. 13:24-30.

1. Mavuno ya mwisho yaja mwishoni mwa ulimwengu, Math. 13:24-30.
2. Hata hivyo, hata katika maisha dhambi zi wazi na zinaadhibiwa, 1 Tim. 5:24.
3. Waovu watateswa katika adhabu ya milele, Math. 25:46; 2 Wathes. 1:7 -10.
4. Wenye haki watang'ara kama jua katika ufalme wa baba yao, Math. 13:40-43.

Mwisho: Njoni tusemezane pamoja, Isa. 1:18, pandeni sasa ili kuvuna na shangwe vije asubuhi, Zab. 125:5-7.

Tukipanda pamoja na Yesu katika mfano wa mauti Yake tutafufuliwa katika mfano wa ufufuo Wake, War. 6:5-7. Anza mavuno ya kiroho sa sa na kupokea taji ya uzima wa miIele wakati huo!

**HUWEZI KUMDANGANYA MUNGU**
Wagal. 6:7-10

Azimio: Huwezi kumdanganya Mungu kwa hiyo acha kujidanganya!

Shabaha: Kutuwezesha kutambua kuwa lazima tutavuna tutakalolipanda.

Dibaji: Kwa wengi maisha ni madanganyo. Kujidanganya ndicho kitu katika ulimwengu chepesi kukifanya. Mtu anavifanya vitu anavyovifanya kuwa vya haki. Watu hupata udhuru ili asikutane na mambo yaliyo ya haki.

Watu huacha kuhudhuria ibada za kanisa kwa sababu: "Wazee hawajahitimu," au "mhubiri analiendesha kanisa," au "hakuna mtu aliye nitembelea nilipokuwa mgonjwa," wengine hukataa kutoa wanavyotakiwa kwa sababu: "mhubiri anazi chukua zote," au "sipendezwi na wanavyozitumia pesa zangu," au "ni kanisa lisilo na urafiki," n.k. Udhuru wo wote utafaa!

Katika mambo ya wema ni sawa: Mlevi anasema, "mimi si mlevi," aliyerukwa akili anasema, "sina shida hasa," au mkristo wa ulimwengu anasema, "kuna wengine wengi wanaofanya mambo mabaya kuliko mimi." Kila mmoja amedanganywa! Mtu, peke yake, katika viumbe alivyoviumba Mungu, anao uwezo wa kuji. danganya kwa makusudi. Biblia mara kwa mara limeonya kuhusu kujidanganya huku, Yak. 1:23-24; 1:26; na Waga1. 6:7-10.

A. "Usiwe Chini Ya Madanganyo: Huwezi Kumdanganya Mungu," 6:7.
  1. Kwani Mungu anawajua wote na kuwaona wote, Math. 6:24-33; Yoh. 2:25; 1 Sam. 16:7; 1 Mambo. 27:9; Yer. 17:9-10.
  2. Kwani Mungu kila siku anayaangalia mambo yaliyo ya kweli tu, 1 Pet. 1: 17; Mdo. 10:24.

B. Mavuno Ya Mtu Yanategemea Hasa Juu Ya Mambo Anayoyapanda, 6:7.
  1. "Apandaye katika mwili - atavuna uharibifu,"
    a. Mtu ni wa mwili, kwa hiyo, kuna mapigano ya daima, Wagal 2:20; 5:24; 6:14; War. 8:12; 1 Pet. 2:11.
    b. Historia ya mtuni ya dhambi: ulimwengu wa kale, 2 Pet. 2:5; Sodoma na Gomora, 2 Pet. 2:6; taifa la Kiyahudi, War. 11:22-24; Sisi leo, Zab. 32:12; 9:17; Mith. 14:34.
    c. Mwisho wa mwanadamu ni wa hakika, 2 Pet. 2: 4; Yuda 6; War. 6: 23.
  2. "Bali yeye apandaye kwa Roho katika Roho atavuna uzima wa milele," 6:8.
    a. Mtu anaweza kushinda, 1 Wakor. 10:13; Wafil. 4:13; Waef. 3:20; War. 8:13.
    b. Mtu katika Mungu anaweza kufaulu! 1 Wakor. 15:57, mtu mmoja na Mungu ni kundi katika kikosi cha mtu yo yote! War. 8:37; Yusufu alifaulu katika Misri; Danieli alifaulu kule Babeli; Esta katika Peresi!
    c. Mwisho wa mtu umehakikishwa, Ufu. 21:1-4.

3. Swali sasa linakuja - Unapanda namna gani? Uwe mwaminifu na huenda ukaishi!

C. "Tusichoke Katika Kutenda Merna Maana Tutavuna Kwa Wakati Wake, Tusipozimia Roho," 6:9-10.

1. Karibuni vitapita, 2 Pet. 3:3-4; 2 Wakor. 4:16-18.
2. Tufanye kazi kungaIi mchana, Yoh. 9:5; Waef. 2:10.
3. Tuchuchumilie kiIa bahati kwa ajiIi ya Mungu, Waef. 5:15-16.
4. "Na hasa jamaaya waaminio! 1 Wakor. 15:33.

Mwisho: Huwezi kumdanganya Mungu, basi kwanini usiache kujidanganya! Utapotea wewe mwenyewe!

**MSALABA WA KRISTO**
Wagal. 6:14

Azimio: Msalaba ndio ulikuwa sababu hasa ya kuwepo kwake Kristo duniani, na ndio moyo na kiini cha maisha ya mkristo.

Shabaha: Kuonyesha nafasi ya msalaba wa Kristo katika maisha ya Krista, injili na katika maisha ya mkristo.

Dibaji: Msalaba wa Kristo ndiyo alama inayotambulikanasana ya Ukristo. Ulikuwa ni kikwazo kwa Wayahudi na upuuzi kwa Mataifa. Lakini kwetu sisi tulioitwa na Mungu, msalaba unasimamia uwezo na hekima ya Mungu.

Katika soma hili tunakusudia kufikiria nafasi ya msalaba katika maisha ya Kristo, katika injili na katika maisha yetu leo.

A. Nafasi ya Msalaba katika Maisha ya Kristo.

1. Msalaba haukuwa kwa ajali, ulikuwa katika nia ya Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, 1 Pet. 1:20; katika Mwa. 3:15 ilikuwa ni ahadi ya kwanza ya msalaba; Taz. pia Zab. 22:16-17; Isa. 53:4-7; 53:12.
2. Kutokana na ubatizo wa Yesu tunajua kuwa alielewa kuwa lazima "atimize haki yate," kwa hiyo aliuvumilia msalaba, Math. 3:13-15. Yalikuwa ni mapenzi ya Mungu kwa Kristo kuwa upatanisho wa dhambi zetu, msalabani, War. 3:25.
3. Akiangalia Yerusalemu Yesu aliuangalia msalaba, Math. 16:21-23.
4. Msalaba huu ulikuwa uwe ndio uwezo wa kuwavuta wanadamu wote, Yoh. 12:32; Ufu. 5:9-16.
5. Yesu alitambua haya ndiyo yalikuwa mapenzi ya Baba, Lk. 22:42-43.
6. Aibu ya msalaba, Math. 27:33-44; Laana ya Sheria, Wagal. 3:13.
7. Katika mauti 'hii msalabani Yesu alijidhiri kwa ajili ya mwanadamu, Wafil. 2: 5-8, akaidharau aibu, Waebr. 12:2. Siku ya kutisha!

B. Nafasi ya Msalaba katika Injili.

1. Msalaba wa Kristo ndio moyo wa neno la injili, Mdo. 2:22-24; 3:18-19; 1 Wakor. 1:17-31; 2:1-2; 15:1-4.
2. Msalaba wa Kristo uliitimiza sheria ya Musa na kuiondoa, Math. 5:17; Yoh. 19:28-30; Waef. 2:14-15; Wakol. 2:14; Waebr. 10:9-10.
3. Msalaba wa Kristo ndio msingi wa upatanisho, Waef. 2:14-18; Math. 26:28.
4. Msalaba wa Kristo ndio msingi wa amani yote, Wakol. 2:19-20.
5. Msalaba wa Kristo ulinunua kanisa, mwili pekee a1ioahidi kuuokoa, Mdo. 20:28; Waef. 5:22-27.

C. Nafasi ya Msalaba Katika Maisha ya Kristo.

1. Msalaba wa Kristo ni wa lazima kwa kuwa Mkristo, War. 6:1-7; kwa kuitii tu "namna" ya kifa cha Kristo, mazishi na ufufuo, tunakuwa "watumwa wa haki," War. 6:16-18.

2. Msalaba wa Kristo ni wa 1azima kwa kuwa wanafunzi, Math. 16:24-26; Ni msalaba wa kubeba "kila siku," Lk. 9:23; Ni msalaba wa "kiIa mmoja binafsi" Lk. 14:27. Kwa hiyo ni "aibu" itakayochukuliwa, ni "aibu ya kila mmoja" itakayochukuliwa, ni "aibu ya kila mmoja ya kila siku" itakayochukuliwa na kila mwanafunzi! Mungu atusaidie!

3. Msa1aba wa Kristo unamsulibisha mtu kwa ulimwengu, Wagal. 6:14, mambo ya dunia hufa Kristo aishipo, Wagal. 2:20. Tamaa kwa ajili ya uovu 1azima zikome, Wagal. 5:24. A. Msalaba wa Kristo hutufungulia njia kwa Mungu sisi watu wenye dhambi, Waebr. 4:14; 5:3; 5:7-9; 7:25; 8:12; 8:27-28.

Mwisho: Msalaba ulikuwa sai kubwa ambalo Kristo alipambana nalo. Ni sai kubwa bado linalopatikana katika ulimwengu leo! lnachukua wanaume na wanawake wenye kujitoa mhanga kubeba msalaba, kwa majivuno hata hivyo kwa upoIe. Kuna chukua ujasiri wa ajabu kuibeba aibu yake. Inachukua uvumilivu mkubwa kuubeba kiIa siku. Hata hivyo bado ni uwezo na hekima ya Mungu! Unangoja utii wako, unangoja kuchukuliwa, bali hatimaye utakuona katika usa1ama nyumbani! Kwanini usikubali leo? Mwana wa Mungu mwenyewe na Malaika walio juu wanangojea kuukubali kwako msalaba wa Kristo!

**www.kanisalakristo.com**
**www.kountzeheath.vox.com**

**SLP 724**
**Mbeya, Tanzania**